
Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

# JARIDA

TOLEO MAALUM LA AGOSTI, 2021

## ZIARA YA MHE. WAZIRI MKUU KATIKA MRADI WA SHAMBA LA MIWA MKULAZI NA KIWANDA CHA SUKARI MBIGIRI







Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

**NSSF**

**Simu Bure 0800116773**

customercare@nssf.or.tz

@NssfTanzania

# WAZIRI MKUU AAGIZA MAKONTENA YENYE MITAMBO YA KIWANDA CHA SUKARI MBIGIRI YALIYOKWAMA BANDARINI YATOKE MARA MOJA

**Na MWANDISHI WETU**

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Watanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, amewaagiza Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Mhe. Jenista Mhagama na Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tixon Nzunda wakutane kwa haraka ili wafanye maamuzi ya utoaji wa makontena 21 yenye mitambo mbalimbali ya ujenzi wa kiwanda cha sukari Mbigiri yaliyokwama katika bandari ya Dar es Salaam.

"Katibu Mkuu (Ofisi ya Waziri Mkuu) upo hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, ndiye anayeisimamia NSSF (Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii) pamoja na mradi huu, Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ndiye mwenye mamlaka na TRA wakutane kwa haraka tunataka kuona makontena yote yanakuja hapa, kiwanda kiendelee kujengwa ili kukidhi lengo la Serikali la kujitosheleza katika mahitaji ya sukari nchini liweze kukamilika," alisema Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu alisema hawataupa nafasi ucheleweshwaji wa mitambo hiyo usiokuwa na ulazima na alimuagiza Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Wenye Ulemavu), Mhe. Ummy Nderiananga kumfikishia salamu Waziri Jenista kwamba wakae na Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Nchemba wafanye maamuzi ya kutoa makontena hayo na taratibu nyingine ziendelee ili ujenzi wa kiwanda hicho usikwame.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba, alisema kupitia ziara ya Waziri Mkuu wamefarijika kutokana na nia ya dhati ya Serikali inayotaka kiwanda hicho kianze kazi ya uzalishaji sukari haraka iwezekanavyo inaonekana.

Naye, Kamishna Msaidizi wa Magereza, Msepwa Abdalla Omar, ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi wa Shirika la Uzalishaji Mali la Magereza, alisema ziara ya Waziri Mkuu imewapa tumaini jipya kwani sasa kiwanda kinaenda kukamilika, uzalishaji utaanza na matarajio ya Serikali pamoja na wabia wa kiwanda hicho ambao ni NSSF na Magereza kupitia kampuni tanzu ya Mkulazi yatapatikana.



Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa (katikati) akielekeza jambo kwa Meneja wa Shamba la Miwa la Mkulazi, Mhandisi Flavian Regonard (kushoto) wakati alipotembelea mradi wa shamba hilo. Kulia ni Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Martin Shigella.

# MAENDELEO MAKUBWA SHAMBA LA MIWA MKULAZI YAMGUSA WAZIRI MKUU









**Na MWANDISHI WETU**

Waziri Mkuu, Mhe. Kassim Majaliwa, ameridhishwa na kazi kubwa ya kutia moyo inayofanywa katika mradi wa shamba la miwa Mkulazi tofauti na alipotembelea kwa mara ya kwanza mradi huo mwaka 2018.

Alisema katika ziara hiyo amekuta mabadiliko makubwa kwenye shamba hilo ambayo yanazidi kuwatia moyo kwa sababu kipindi cha nyuma kulikuwa hakuna ofisi na mara ya mwisho alipotembelea mradi huo mwaka 2018 alikuta jengo moja ambalo lilikuwa linajengwa lenye sura ya mbawa za ndege, lakini sasa kuna majengo mengi pamoja na ofisi mzuri ambazo zimekamilika.

Waziri Mkuu alisema mradi huo ni muhimu kwa Watanzania wote ambao ulibuniwa mwaka 2016 na unaendeshwa kwa ubia baina ya Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Jeshi la Magereza kupitia Kampuni Hodhi ya Mkulazi.

Mwenyekiti wa Bodi wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi, Dkt. Hildelitha Msita alisema hatua iliyofikiwa sasa katika shamba hilo ni kubwa ambapo ekari 2,705 zimeshapandwa miwa na kwamba kiwanda kinajengwa hatua ambayo inaenda kuleta mwanga wa kumaliza ama kupunguza uhaba wa sukari nchini ambapo ndani ya mwaka mmoja ujao wataanza kuzalisha sukari.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Mhe. Martin Shigela, alisema alifanikiwa kutembelea na kuzungumza na wananchi ambapo moja ya changamoto kubwa katika eneo hilo ni ardhi na kwamba changamoto hiyo wanaendelea kuitatua kwa kuwapatia ardhi ambayo Mhe.Rais Samia aliwasaidia kuipata baada ya kufuta hati za awali za mashamba hayo.

# ZIARA YA WAZIRI MKUU MKULAZI, MBIGIRI KATIKA PICHA


















# VIJANA WAZALENDO WAHAMASIKA KUPATA MAFUNZO YA KUENDESHA MITAMBO YA KIWANDA CHA SUKARI MBIGIRI

**Na MWANDISHI WETU**

Ujenzi wa kiwanda cha sukari Mbigiri mkoani Morogoro umeibua fursa kwa vijana wazalendo wa Kitanzania ambao wamehamasika kupata mafunzo ya kuendesha mitambo ya kiwanda hicho kuanzia mwanzo wa ujenzi mpaka kitakapokamilika.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti baadhi ya vijana waliopata kazi katika ujenzi wa kiwanda hicho, waliishukuru Serikali kwa kupata fursa hiyo ya kujifunza kuendesha mitambo kutoka mwanzo wa ujenzi wa kiwanda chenyewe mpaka wakati wa kufunga mitambo hiyo mpango ambao ni mzuri.

Joseph Marua, ambaye ni Afisa Utawala wa Kampuni ya BQ Contract Limited, alisema kupitia mradi huo wa ujenzi wa kiwanda cha sukari, kampuni yake imeshatoa ajira kwa vijana wapatao 60 ambapo aliishukuru kampuni ya Mkulazi kwa namna ilivyotoa fursa kwa vijana wazawa kuweza kufanya kazi katika mradi huo ambao ni muhimu kwa uchumi wa nchi kwa ujumla.

Naye, Frenk Nyari ambaye ni miongoni mwa vijana waliopata ajira katika mradi huo, aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita kwa namna inavyousimamia mradi huo ambao umeshatoa ajira kwa vijana wazawa na wanafanya kazi kwa moyo mkubwa kwani baada ya kukamilika utatoa ajira nyingi zaidi.

Kwa upande wake, Jonas Steven alisema kupitia mradi huo vijana wengi watapata ajira na ameahidi kufanya kazi kwa bidii na maarifa ili mradi uweze kuleta tija na kutimiza lengo kusudiwa.

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), Masha Mshomba, alisema NSSF na Jeshi la Magereza ndio wamiliki wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi, ambapo kupitia ziara hiyo ya Waziri Mkuu alitoa msisitizo wa kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu katika kulima miwa na shughuli nyingine ambazo zinaendana na mradi huo ili waweze kunufaika kikamilifu.






# NUKUU MUHIMU



"Katibu Mkuu (Ofisi ya Waziri Mkuu) upo hapa, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ndiye anayesimamia NSSF pamoja na mradi huu, Waziri wa Fedha na Mipango ambaye ndiye mwenye mamlaka na TRA wakutane kwa haraka tunataka kuona makontena yote yanakuja hapa na kiwanda kinaendelea kujengwa ili kukidhi lengo la Serikali la kujitosheleza katika mahitaji ya sukari nchini liweze kukamilika."

**Mhe. Kassim Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



"Hatua iliyofikiwa sasa katika shamba hili (Mkulazi) ni kubwa ambapo ekari 2,705 zimeshapandwa miwa na kiwanda kinaenda kujengwa hatua ambayo inaenda kuleta mwanga wa kumaliza ama kupunguza uhaba wa sukari nchini."

**Dkt. Hildelitha Msita, Mwenyekiti wa Bodi wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi**



"Tunaishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kupitia kwa Waziri Mkuu aliyeagiza yale makontena yenye vifaa vya viwanda yatolewe mara moja bandarini na shughuli za ujenzi ziendelee. Hili ni jambo kubwa na zuri sana kwetu sote."

**Masha Mshomba - Mkurugenzi Mkuu NSSF**



"Ziara hii imetupa tumaini jipya kwani sasa kiwanda kukamilika, uzalishaji utaanza na matarajio ya Serikali pamoja na wabia wa kiwanda hicho ambao ni NSSF na Jeshi la Magereza kupitia kampuni tanzu ya Mkulazi yatapatikana."

**Msepwa Abdalla Omar, Kamishna Msaidizi wa Magereza**



"Tunaishukuru Serikali kwa kutupa fursa ya kujifunza kuendesha mitambo kutoka mwanzo wa ujenzi wa kiwanda chenyewe mpaka wakati wa kufunga mitambo hiyo mpango ambao ni mzuri."

**Joseph Marua, Afisa Utawala wa Kampuni ya BQ Contract Limited**

# SERIKALI YABAINISHA FURSA UWEPO SHAMBA LA MIWA MKULAZI, UJENZI WA KIWANDA CHA SUKARI MBIGIRI



**Na MWANDISHI WETU**

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amesema pamoja na mipango ya Serikali kuimarisha sekta ya kilimo na zao la miwa kwa ajili ya kuzalisha sukari walifanya maamuzi ya kuanzisha miradi mikubwa ukiwemo wa shamba la miwa Mkulazi ambao unawahusisha wananchi ili waendelee na kilimo.

"Ardhi yenu ni nzuri kwa miwa na (nyinyi) mpo hapa ni vizuri mkalima kulingana na mahitaji ya ardhi mliyo nayo, tumeleta kampuni hii (Mkulazi) ambayo inamilikiwa kwa ubia baina ya NSSF kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu na Jeshi la Magereza," alisema.

Waziri Mkuu alisema inaendelea kuratibu kwa kushirikiana na watendaji wa Kampuni ya Mkulazi ili kuona namna ya kusaidia kilimo cha miwa ili kiwe rahisi zaidi kwa wakulima kupata mashamba, usafirishaji, mbegu na maji ili wananchi nao wawe wazalishaji wakubwa wa miwa.

Mtendaji Mkuu wa Kampuni Hodhi ya Mkulazi, Selestine Some, alisema walifanya kikao na wakulima wa miwa ambao walikuwa na changamoto ya magari kuweza kuingia katika mashamba yao lakini kampuni ilichukua vifaa vyake kukwangua kilomita 12 za barabara ili kusaidia miwa itolewe shambani.

Kwa upande wao, Mbunge wa jimbo la Mikumi, Mhe. Denis Lazaro na Mbunge wa jimbo la Kilombero Abubakar Daniel Asenga waliipongeza Serikali kwa jitihada ambazo inazoinesha kwa wakulima wa zao la miwa.



BOARD OF TRUSTEES
NSSF
NATIONAL SOCIAL SECURITY FUND

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

Tunajenga Maisha Yako
ya Sasa na Baadaye

NSSF